



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Wednesday, 19th November, 2025

Third Assembly – Fourth Session
SEVENTY FOURTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:30p.m at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Good afternoon, Members.

STATEMENT(S)

RESPONSE TO STATEMENT BY CHAIRPERSON COMMITTEE ON IMPLEMENTATION HONOURABLE
SAMUEL MWAURA ON THE STATUS OF IMPLEMENTATION ON MOTION ON ACCESSIBILITY OF
BUILDINGS BY PERSONS OF DISABILITIES

Yes, Honourable Samuel Mwaura? Any Member from Implementation Committee? Yes, Honourable Leila on behalf of Honourable Mwaura I think I saw him maybe he has gone to the washrooms.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi pia ni mmoja katika Kamati ya Utendaji; naomba mtupatie mda manake ilikuwa ripoti na majibu yalikuwa tayari, lakini hayajafika pale kwa Makatibu. Kwa hivyo naomba na haijaingia kwa *House Business* na naomba kama itawezakana uweze kutatupatia mda kidogo manake saa hizi tunaenda mapumzikoni pia, hapo tutakapo rudi tutaleta ripoti kamili. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. The matter will be returned back to the House Business to be sorted for another day. Yes, Clerk.

PROCEDURAL MOTION

ADJOURNMENT OF THE COUNTY ASSEMBLY FOR THE 2025 CASA GAMES

Yes, Leader of Majority Honourable Athman Mwamwiri?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 1*

THAT, pursuant to the provision of Standing Order 28(1), this County Assembly do now adjourn to allow Members and staff to participate in the County Assemblies Sports Association (CASA) Games scheduled from 22nd to 28th November, 2025, and that the Assembly resumes its regular sittings on Tuesday, 2nd December, 2025.

May I ask Honourable Kibwana Swaleh to second the Motion?

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Kibwana?

Hon. Kibwana Swaleh: Thank Honourable Speaker, Mr. Speaker, I do second.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Members I now propose a question that, the Procedural Motion on Adjournment of the County Assembly for the 2025 CASA Games be debated in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Athman Rama Mwamwiri?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, the adjournment is on a calendar event which we as the Members and the staff of the County Assembly, do hereby participate in each and every year. Mr. Speaker, the CASA Games which unites and brings together all the 47 Counties in a supposed extravaganza so all of us here Members and staff, we are prepared for the games. Therefore, I seek and urge all the Members to agree that we adjourn so that we can finalize on our preparations before we travel to Meru for the big event. And also, Mr. Speaker, I give a disclaimer to Members that Meru is the home of *Miraa* so, let us go and focus with the games and not on the other business. So, I urge all the Members Mr. Speaker, we agree upon and finalize our preparations so that we can go and guard our emblem, our County, our Assembly in this extravaganza. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mwalimu Kambi, Juma.

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu kwa sababu tumejitayarisha vilivyo kwa michezo tofauti. Kwa hivyo tuko tayari kwenda kupambana, na safari hii kile kikosi changu cha *choir* kitaleta kikombe katika Kaunti yetu ya Mombasa. Ahsante sana kwa nafasi hii.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, the netballer in the House Honourable Leila Nyache.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika tena kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja ilioletwa na Kiongozi wa Wengi Mheshimiwa Mwamwiri. Napongeza hoja hii kwa sababu sasa hivi tunaenda kwenye michezo na inahitaji tupumzike ndio tuweze kufanya mazoezi vizuri tukiingia kwa michezo tuwe ni washinde. Kwa mfano sisi ma *netballers* mimi ndio *shooter* niko na mwenzangu ma *shooter* ndio sisi wenye kufunga magoli ndio sisi. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi nafurahi nikifanya haya mazoezi kwa sababu inasaidia pia viungo vya mwili, inasaidia kupunguza maradhi katika afya zetu na unaona bado Mheshimiwa

Leila anaita kwa sababu ya hayo mazoezi. Kwa hivyo mimi nashukuru na naomba wenzangu waweze kuchangia tuweze kwenda mapumzikoni na twende Meru tukafanye michezo yetu na tunaomba turudi na ushindi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Florence.

Hon. Kachumbo: Thank you, Mr. Speaker for this opportunity. I stand to support the Motion. I agree with my colleague Honourable Leila we are both in netball, and it's a good time for Honourable Members to exercise. This will be beneficial for their health and for the staff also because they have been committed to work and now it is time to have a break. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Jactone Madialo.

Hon. Madialo: Thank you, Honourable Speaker. Honourable Speaker...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Madialo proceed.

Hon. Madialo: Thank you, Honourable Speaker. Whereas, as I stand here to support this Motion, I was a bit wondering why the Majority Leader while questioning Members about Meru being a Miraa growing zone, his eyes were fixated on Honourable Leila. Now, further, I would also like to add to the research that currently Meru has surpassed Homa Bay as the County with the highest prevalence of HIV and AIDS. Thank you, Mr. Speaker Sir.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Matsaki Morgan?

The Leader of Minority (Hon. Matsaki): Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Mimi pia nasimama kuunga mkono wacha Kaunti hii 001 ikawakilishe vilivyo na matumaini tutakapofika pale tutakuwa washindi kwanza *especially tag of war* tuko na baba mjengo Mheshimiwa pale najua tuko pamoja. Kwa hivyo nimesimama pia kuunga mkono. Ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you, Honourable Matsaki. Yes, Honourable Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Mheshimiwa Spika sisi Mwenyezi Mungu ametujalia hasa mimi nikiwa na kipaji changu urasmi cha kuwa mimi ni *goalkeeper* na huu ugolikipa wangu hauwezi kuwa na fursa kama itakuwa mimi sina timu na naunga mkono hoja hii kwa sababu *goalkeeper* katika Bunge la Kaunti hii ya Mombasa si mwengine isipokuwa ni mimi Hamisi Salim Mbaya na kwa sababu hiyo na waahidi Waheshimiwa wenza tutakapokwenda kwenye michezo tunayoenda kuwakilisha Bunge letu la Mombasa hakuna bao litapenya...

[Applause]

Kwa sababu nitakuwa niko imara kwenye goli Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja hii nikikuhakikishia kuwa ushindi tutakuja nao kama timu Mheshimiwa Spika. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Ojala?

Hon. Ojala: Thank you, Mr. Speaker once again for giving me this opportunity. Mr. Speaker, I stand to support the Motion at the adjournment of the County Assembly for the 2025 CASA games. Mr. Speaker, I stand to support the Motion I find it very interesting for the Member of Mikindani to say that Honourable Majority Leader Athman Mwamwiri was referring to Leila, as you are aware in this Honourable Member majority are victims and the Majority Leader did not refer to the Honourable for Kipevu Honourable Leila, Mr. Speaker. I was consulting with the Majority leader because I heard Honourable Member of Timbwani saying he is a goalkeeper, which is very right but I wanted to know the term of a goalkeeper in Kiswahili and today I'm very proud to know when you say a goalkeeper in Kiswahili, *ni mlinda lango* I think I'm good now to go in Kiswahili, Mr. Speaker. Thank you. I stand to support.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mwaura? What is it, Honourable Madialo?

Hon. Madialo: Is Honourable Ojala in order to say that I expressly indicated that the Majority Leader was referring to Honourable Leila! I said that while he was executing his point, his eyes were fixated on Honourable Leila. That does not mean he was referring to Honourable Leila as a Miraa chewer I simply said that while he was executing his point his eyes were fixated. Maybe he was admiring Honourable Leila. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Okay, thanks, Honourable Madialo. Yes, Honourable Leila, what is it?

Hon. Nyache: Mheshimiwa Spika naomba kurekebisha hapo wasininukuu vibaya mimi na mambo ya kutafuna Miraa na nini siko! Mimi Mheshimiwa Leila siko kabisa!...

[Applause]

Siko kabisa!

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you.

[Interruption]

Hon. Nyache: Hapo wanitoe.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you, Honourable Leila. You are just chewing gum.

Hon. Nyache: Labda *chewing gum* lakini hii mambo ya miraa sijui mambo ya *Mugoka* mimi siko kabisa!

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Okay, Honourable Mwaura, then Honourable Mwamwiri.

Hon. Mwaura: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa nami pia nichangie kwa hoja hii, ambapo ninaiunga mkono hoja hii ya kuenda mapumzikoni kwa muda mchache ili sisi pia tuende tukasisimue misuli na pia tuende tukaleta ushindi kwa michezo yote ambayo tutakuwa tukicheza ikiwa mimi hapa nitakuwa nikirusha mishale almaarufu darts kwa wale wanaofahamu. Nitakuwa ninarusha mishale ya *darts*. Mishale ya *darts* inarushwa na wale ambao wanajua kupima na kulenga vizuri na hiyo ndiyo kazi ambayo nitakuwa ninafanya kule. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Athman Rama Mwamwiri, please reply to the Motion the Majority Leader.

The Majority Leader (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, nifarijike ya kwamba Waheshimiwa licha ya kuunga mkono hoja hii, lakini pia wako katika ari *bam bam*, ya kushiriki michezo hii, ishara ya kwamba hatutaenda kimatembezi lakini tutaenda kuwakilisha Gatuza letu la Mombasa na Bunge la Mombasa katika michezo hii. Mheshimiwa Spika, ari hii pia inatuhakikisha ya kwamba safari hii ushindi ni wetu wana Mombasa japo Mheshimiwa Spika nina masikitiko ya kwamba yule mlinzi mwenza wako katika safu ya ulinzi Mheshimiwa Madialo, siku hizi amekataa kupunguza uzani na sioni kama atapata namba katika timu ya kandanda lakini pia nipongeze Waheshimiwa wote kwa kuweza kujumuika katika mazoezi haya pamoja na wafanyi kazi wetu, kuweza kujikurubisha kwa ukaribu zaidi, kutangamana zaidi bali na mazingira mazito ya kuhakikisha wananchi ya kazi hii yetu lakini pia tunapata wasaa wa kufanya mazoezi pamoja, kucheka pamoja, kujenga udugu na tunasafiri kama familia.

Mheshimiwa Spika na ni wito tu ya kwamba kama timu yako haikuwa katika uwanja kwa wakati ule, basi sote kwa pamoja twende kumshabikia Mheshimiwa Mwaura akirusha mishale japo awali, michezo hii ilikuwa ikinasibishwa sana na walevi lakini siku hizi vijana pia wanaicheza michezo hii. Pia nifarijike kuwa Mheshimiwa Leila ametuhakikishia ya kwamba ule ushabiki na uraibu yeye hayumo na nimsihi tu ya kwamba mchezo yetu ya pete inapofika masaa ya mchana hupata dhiki sana Mheshimiwa Leila kutufungia magoli, apite hospitali mapema, abadilishe miwani ilijua likiwa kali miwani yake iweze kumsaidia kutuwekea yale mabao kwa sababu huwa ni tegemezi katika timu yetu ya pete Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa wote na wafanyikazi wote wa Bunge niwatakie safari njema, tukajumuike kwa furaha tujitume kwa ajili ya jina la Bunge letu na turudi nyumbani wazima Mungu atuwezeshe tukiwa na ushindi na vigelegele kwa ushindi huo. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Honourable Members, I now stand to put the question that the Motion by the Leader of the Majority on adjournment of the County Assembly for the 2025 CASA games be approved in this Honourable House in the same terms as debated.

[Question put and agreed to]

Honourable Members, the Motion by the Leader of Majority Party on the adjournment of the County Assembly for the CASA games, 2025 is adopted by the House. Yes, Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, the House stands adjourned until Tuesday 2nd December, 2025 at 10:00a.m.

The House rose at 2:50p.m.